# HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA

SHULE YA SEKONDARY NDELA,
S.L.P 19,
**MBINGA.**
..../......./20....

Kumb.Na................................

JINA LA MWANAFUNZI.........................................................

SHULE ANAYOTOKA................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2021**

1.0. UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondary Ndela.Napenda pia kuchukua nafasi hii kukupongeza na kukukaribisha hapa shuleni.Nimategmeo yangu utasoma kwa bidii ili ukishapata Elimu ya sekondari uweze kumudu na kufurahia maisha yako.

Shule ya Sekondari Ndela ipo katika kata ya Utiri kaskazini mashariki ya Mji wa Mbinga kando ya barabara kuu ya Mbinga-Songea kilometa 5 toka kwenye kituo cha mabasi cha Mwembe na kilometa 2.5 toka Mtama.Ni shule ya kutwa na ya mchanganyiko.

Shule itafunguliwa siku ya Jumatatu tarehe 11/01/2021 .Unatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo ili kuanza masomo mara moja.Usisahau kuja na fomu ya Afya na ile ya ahadi ya kutimiza wajibu zikiwa zimekamilika.

Ukiwa hapa Shuleni utajifunza masomo ya Uraia,Historia,Jiografia,Kiswahili,Kiingereza, Hisabati,Fizikia,Kemia,Elimu ya viumbe na dini.Ukiachana na Kiswahili na Dini masomo mengine yote yanafundishwa kwa lugha ya Kiingereza.Ili uyaelewe vizuri masomo haya, unapaswa kuitumia lugha ya Kiingereza wakati wote uwapo hapa Shuleni

## 2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Ili uweze kusoma kwa ufanisi,ukiwa hapa shuleni unapaswa kuwa na vifaa,Vyombo muhimu na pia kuzifahamu kanuni na sheria zinazohusiana na maisha ya shule ikiwa ni pamoja na kukamilisha mambo mengine ya msingi ili usisumbuliwe utakapo kuja kuanza masomo.

Ufafanuzi wake wa kina unapatikana kwenye vipengele vinavyofuata. Tafadhali visome kwa umakini na kuvielewa ipasavyo:-

## 2.1. SARE YA SHULE

### 2.1.1 WAVULANA

(i). Suruali mbili rangi ya ***UGORO DARK****(Isiyobana)* aina ya ***ISTIMU*** (*Namba moja*)

(ii). Shati mbili nyeupe mikono mifupi

(iii). Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vyenye visigino vifupi

(iv). Soksi rangi nyeupe

(v). T-shirt rangi ya bluu Bahari, Track na raba kwa ajili ya michezo

### 2.1.2. WASICHANA

(i). Sketi mbili rangi ya ***UGORO DARK***(*ndevu inayoguza soksi*) aina ya ***ISTIMU*** (*namba moja*)

(ii). Shati mbili nyeupe mikono mifupi

(iii). Soksi rangi nyeupe

(iv). T-shirt rangi ya bluu Bahari, Track na raba kwa ajili ya michezo

(v). Viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili

## 2.2. VYOMBO NA VIFAA KWA WOTE

(i). Kalamu za wino na risasi

(ii). Mkebe wa hesabu (mathematical set)

(iii). Jembe jipya lenye mpini, fyekeo na ndoo ya lita 10

(iv). Madftari makubwa (Counter book)12 na zaidi

(v). Sweta rangi ya bluu iliyoiva lenye shingo ya V

(vi). Vitambaa viwili vya mfukoni (Leso)

(vii). Kamusi/ Dictionary (English – Swahili)

(viii). Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli,kikombe na kijiko)

## 3.0 . KANUNI NA SHERIA ZA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzisoma sheria hizi kwa umakini, kuzielelewa na hatimaye kuzitekeleza. Kuzikiuka kutasababisha mambo yasiende ipasavyo hapa shuleni na hata

kuiletea shule sifa mbaya. Hivyo basi, hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wale watakaozikiuka.

## 3.1. WANAFUNZI

(a). Wasimame na kumsalimu yeyoste anayewazidi umri unapopita, kuingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

(b). Waonyeshe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote wawapo

(c). Sharti wamsalimie mwalimu au mtu yeyote anayewazidi umri anapopita ua kuingia mahali walipo.

(d). Wawaheshimu wafanyakazi wote kama wazazi na walezi wao.

(e). Wasitumie lugha mbaya wakati wowote, kati yao wenyewe kwa walimu na kwa watu wengine.

(f). Washirikiane,kupendana na kusadiana wao wenyewe katika mambo mbalimbali pia wathamini na kuziheshimu kazi za aina zote.

(g). Wathamini na kuheshimu mali binafsi na zile za umma na kuzitunza.

(h). Wathamini muda wa kuwahi katika shughuli zote zilizomo kwenye ratiba ya kila siku. Kila mmoja awahi na kuhudhuria wito wa dharura (emergency) waitike wito au ishara yoyote ya kuwaita bila kuchelewa.

(i). Waheshimu bendera ya Taifa,picha za viongozi wa serikali,nembo ya Taifa wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.

(j). Wanapokuwa darasani, kwenye mikutano n.k wanyooshe mikono juu na kusimama wanapouliza au kujibu swali.

(k). Wakae kimya wakati wote wanapokuwa madarasani,wasitoke nje bila ruhusa ya Mwalimu au kiongozi aliyepo.

### 3.2.1. IWE NI MWIKO KWA MWANAFUNZI KUFANYA YAFUATAYO:-

(i). Kuvuta sigara ya aina yoyote.

(ii). Kushiriki katika aina yeyote ya ulevi.

(iii). Kufuga ndevu, kucha ndefu, kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi kupaka inna, wanja na kunyoa nyusi.

(iv). Kuvaa mavazi yasiyo na heshima

(v). Kugombana na kupigana

(vi). Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa

**3.2.2. KUTEMBEA SEHEMU ZIFUATAZO ISIPOKUWA KWA KIBALI MAALUMU**

(i). Chumba cha walimu na ofisi za shule

(ii). Maabara

(iii). Jikoni

(iv). Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

**3.2.3. KUTOHUDHURIA**

(i). Vipingi vya masomo ndani na nje ya darasa

(ii). Michezo na kazi zozote za mikono

(iii). Baraza la shule , kupandisha bendera ya Taifa , ukaguzi wa usafi n.k

(iv). Maandalizi ya masomo ya jioni (preparation)

**3.2.4. NI MWIKO KABISA KUTEMBELEA/KUONEKANA SEHEMU ZIFUATAZO**

(i). Vilabu vya pombe

(ii). Majumba ya starehe

(iii). Majumba ya kufikia wageni (*Guest House*).

**3.3. YAFUATAYO NI MAKOSA UKITHIBITISHWA KUYATENDA YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.**

(i). Wizi

(ii). Uasherati, ubakaji, ushoga na ulawiti

(iii). Ulevi na kushiriki biashara ya madawa ya kulevya

(iv). Makosa ya jinai

(v). Kupigana/ kumpiga mwanafunzi mwenzako, mwalimu au mfanyakazi asiyekuwa mwalimu

(vi). Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine

(vii). Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule

(viii). Kutoa au kushawishi utoaji mimba.

(ix). Kuoa au kuolewa ukiwa bado mwanafunzi

(x). Kudharau bendera ya Taifa au wimbo wa Taifa

(xi). Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule.

(xii). Kukataa adhabu kwa kosa ulilotenda au kushawishiwa kutenda.

(xiii). Utoro wa muda mrefu.

(xiv) Kumiliki au kutumia simu ukiwa katika mazingira ya shule

(xv). Kuvaa suruali inayobana, mlege, shati fupi, kuweka mapambo kucha kuwa na nywele ndefu n.k.

## 4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

i. **Fomu ya Afya kutoka kwa daktari wa Wilaya/Halmashauri.**

ii. **Fomu ya Ahadi ya kutimiza wajibu**

## 5.0. HITIMISHO

Hakikisha unashirikiana vema na Walimu na wanafunzi wenzako ili kufanya shule yetu iwe kioo na mahali pazuri zaidi pa kujifunza na kukua kielimu,kimaadili na kinidhamu.Toa taarifa ofisi ya mkuu wa shule mapema iwezekavyo pale unapoona unashindwa kufikia malengo yako ili uweze kupate ushauri wa namna ya kutatua changamoto zinazoweza kukukabili.

**KARIBU SANA**

HEADMASTER
NDELA SEC. SCHOOL
P. O. BOX 19 MBIN...

**Adeline Mandera**

**MKUU WA SHULE**

**SIMU N0: 0756014562**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT OFFICE,REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.

MBINGA TOWN COUNCIL

DATE……/……../20….

TO:

**The Medical officer**

…………………………………

…………………………………

**RE:REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine ……………………………………………as his/her physical and mental fitness for admission as a form **ONE** student at **Ndela SecondarySchool.**

Your sincerely

…………………… HEADMASTER NDELA SEC. SCHOOL P.O. BOX 19 MBINGA

**THE HEADMASTER**

**The Headmaster;**

I have examined the above mentioned student and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full course of secondary school.

1. Blood pressure…………Hemoglobin…………Blood group……………
2. Eyes; Visually acuity with/without glasses: Right………………… Left……………………
3. Hearing: Right ear……………… Left ear……………
4. Throat…………Nose……………Speech……………
5. Respiratory System (a) TB…………….(b)Asthma……….
6. CVS (a) Any congenital art disease……….
7. GIT (a) PUD………………(b)Stool………………
8. GUS (a)Veneral Diseases(VDRL)……………………(b)Urinalysis……………
9. RES (a)Skin Diseases……………..(b)Any allergy…………………
10. MMS (a)Any Deformity…………………(b)Any chronic illness of the joints……………
11. Are there any serious disease e.g Leprosy,Epilepsy,Diabetes?Specify………………………………
12. General comments……………………………………………………………………………………

**DATE**…………………………**STATION**……………………………**SIGNATURE**……………………………

**DESIGNATION**……………………………

Approved by:

…………………………………… ……………………………

**TOWN MEDICAL OFFICER** **DATE**

**MTC**